

Kumiliki nyumba kwa mpango wa Habitat for Humanity

Ni vigumu kwa familia yenye mapato chini ya asilimia 50 ya maeneo ya wastani ya mapato kumiliki nyumba katika East King County. Karibu robo ya familia za Eastside hulipa zaidi ya asilimia 30 ya mapato yao kwa ajili ya makaazi; msongomano na hali ya maisha duni ni kawaida.

Habitat for Humanity of East King County huwajengea nyumba familia zenye zinamapato ya chini, wanao hitaji makaazi nafuu. Familia zenye zimechaguliwa kufanya na Habitat for Humanity lazima kukamilisha usawa (ya ujenzi wa nyumba zao na nyumba ya jirani yao) na kuhudhuria mafunzo ya wanunuzi nyumba kabla kununua nyumba zao kwa asilimia sufuri ya riba.

Ili kushiriki kwa mipango ya umiliki wa nyumba, waombaji lazima kutimiza masharti yafuatayo:

1. Uraia

- Kuishi au kufanya kazi katika King County kwa angalau mwaka mmoja wakati wa kutuma ombi.
- Kuwa wakaazi wa kudumu au raia wa Marekani wakati wa kutuma ombi.

2. Haja

- Msongamano (watu watatu au zaidi kwa chumba kimoja cha kulala).
- Mpito au hali ya makaazi ya muda.
- Makaazi duni (ukosefu wa mazingara bora)
- Kulipa kiasi kikubwa zaidi ya asilimia thelathini ya mapato kungaramia kodi.

3. Uwezo wa Kulipa

- Pato maalum na ambalo litatosheleza kulipa nyumba, gharama ya HOA, ushuru na kodi (takriban jumla ya \$750-\$800 kwa mwezi).
- Mapato chini ya asilimia 50 ya maeneo ya wastani (tazama chati hapa chini)

Jumla ya Mapato ya Familia	
Familia ya watu 6	\$48,900
Familia ya watu 5	\$45,500
Familia ya watu 4	\$42,150
Familia ya watu 3	\$37,950
Familia ya watu 2	\$33,700
Familia ya mtu 1	\$29,500

4. Kujitolea

- Kufanya kazi masaa mia na tano ya ujenzi wa nyumba yako au mradi mwingine.
- Kushiriki katika mafunzo ya kumiliki nyumba, kama vile bajeti na kukarabati nyumba.
- Kuwakilisha Habitat for Humanity katika jamii.

5. Mnunuzi wa nyumba kwa mara ya kwanza

- Wanaotuma ombi la kumiliki nyumba za Habitat wawe hawajawahi kumiliki nyumba kwa miaka mitatu iliopita.

Kwa habari zaidi, pata katika mtandao www.habitatekc.org, simu 425-869-6007, au tuma barau pepe efortman@habitatekc.org